

K.E.Y.E.A

ZANA YA TATHMINI YA UTAYARI WA SHULE NCHINI KENYA

MUHULA WA 2: TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA 2026

GREDI YA 2- KISWAHILI

Muda: Saa 1

TAARIFA ZA MWANAFUNZI



Jina: _____

Shule: _____

Nambari ya Uandikishaji: _____

Tarehe: _____

KWA MATUMIZI YA MPIMAJI

SEHEMU	% ALAMA	Kuzidi matarajio	Kufikia matarajio	Kukaribia matarajio	Chini ya matarajio	Maoni ya mpimaji
KIWANGO		80-100	50-79	40-49	1-39	
Kiwango		4	3	2	1	
Weka tiki kiwango						

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. 1) UFAHAMU

Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo

Zedi ana Ngamia na Punda. Wanyama hao ni wa nyumbani. Wazazi wa Zedi hutumia Ngamia na Punda kwa usafiri. Zedi anaogopa kupanda wanyama hao akiwa peke yake. Akiwa na mtu mzima anaweza kupanda ngamia na punda. Wazazi wa Zedi wanawatunza wanyama hao ipasavyo.

- Ni wanyama gani wametajwa katika hadithi? ____na ____
- Wanyama hao hutumika kwa ____ (ukulima, Usafiri)
- Zedi anaogopa kufanya nini? ____
- Wazazi wa Zedi _____ wanyama hao. (huwatesa, huwatunza)

2. **Soma hadithi kisha ujibu maswali yafuatayo**

Halima na Abdi ni marafiki wa chanda na pete. Wao hucheza pamoja. Wanaenda shuleni pamoja na wanasoma katika darasa moja. Halima anapenda kuchora naye Abdi anapenda kucheza kandanda. Wao huenda kuogelea pamoja. Wote walipata medali ya dhahabu katika mashindano ya kandanda na kuchora.

- _____na _____ ni marafiki wa chanda na pete.
- Ni nini wao hufanya kwa pamoja ? _____

c) Abdi anapenda kufanya nini? _____

d) Wote walipata medali ya aina gani? ___(Dhahabu, Dhehebu, shaba)

3. **Andika maneno yafuatayo vizuri.**

Mfano: **riga - gari**

a) gende - _____

b) lime - _____

c) siba - _____

4. **Andika maneno yafuatayo kwa wingi.**

Mfano: Basi hili - Mabasi haya

a) Gari hili - _____

b) Baisikeli hii - _____



5. **Chagua jibu sahihi kukamilisha sentensi.**

a) Malori _____yamebeba mizigo. (yetu, zetu)

b) Pikipiki _____imeng'ara. (yangu, changu)

c) Mzigo _____ni mzito. (langu, wangu)

6. **Andika jina la wanyama hawa.**




7. Tumia alama ya kiulizi panapofaa katika sentensi zifuatazi.

a) Leo ni siku gani

b) Je, unaitwa nani

8. Andika jina la chombo cha usafiri kisha upake rangi.



9. **KUANDIKA.**

Andika sentensi tano zitakazotamkwa na mwalimu

1. _____
2. _____
3. _____
4. _____
5. _____

